
FAHAMU HAKI ZAKO

Makosa ya Chuki

TUME YA HAKI ZA BINADAMU JIJI LA IOWA

410 E. Washington St.
Iowa City, IA 52240
www.icgov.org/humanrights
356-5022 au 356-5015
humanrights@iowa-city.org

KUPATA FURSA SAWA NA
KUTOBAGULIWA NI SHERIA NA NI HAKI YAKO
Ikiwa unaamini kwamba umebaguliwa, au ikiwa
ungependa kupata maelezo zaidi kuhusu aina za
ubaguzi uliopigwa marufuku, tafadhali wasiliana na
Mshirikishi wa Haki za Binadamu kupitia 356-5022 au
Mchunguzi wa Haki za Binadamu kupitia 356-5015.

©2016

JE, NINA HAKI ZIPI?

Watu walio katika mipaka ya jimbo la lowa wana haki ya kutotendewa virugu, au kutishiwa vurugu, wao binafsi au mali zao kwa sababu ya kabila, rangi, dini, ukoo, nchi walipotoka, msimamo wa siasa, jinsia, mwelekeo wa jinsia, umri au ulemavu. (Kanuni za lowa 729A.1)

MAKOSA YA CHUKI NI NINI?

“Kosa la chuki” ina maana ya mojawapo ya makosa haya ya umma yanapofanywa kwa mtu binafsi au mali yake *kwa sababu* ya kabila la mtu huyo, rangi, dini, ukoo, nchi alikotoka, msimamo wa siasa, jinsia, mwelekeo wa jinsia, umri, au ulemavu, au uhusiano wa mtu huyo na mtu mwingine wa kabila, rangi, dini, ukoo, nchi nyingine, msimamo wa siasa, jinsia, mwelekeo wa jinsia, umri, au ulemavu:

Kumshambulia mtu ni kinyume cha haki za mtu binafsi chini ya sehemu ya 708.2C ya Kanuni za lowa;

Ukiukaji wa haki za mtu binafsi zilizo chini ya Kanuni za lowa 712.9;

Jinai iliyodhamiriwa ya ukiukaji wa haki za mtu binafsi chini ya Kanuni za lowa 716.6A;

Kuingia bila idhini ili kukiuka haki za mtu binafsi zilizo chini ya Kanuni za lowa 716.8.

JE, MTU ANAWEZA KUCHUKUA HATUA ZIPI ILI KURIPOTI KOSA LA CHUKI?

- Wasiliana na walinda usalama.

SULUHU ZA KIRAIA

Mtu ambaye amepata madhara ya kimwili, hisia au kifedha kwa sababu ya ukiukaji wa sura hii kwa kutendewa makosa ya chuki ana haki na anaweza kudai kukomeshwa kwa dhuluma hizo, kudai fidia ya jumla au maalum, kudai ada za wakili na gharama. Shauri linalofunguliwa kwa kuzingatia sehemu hii sharti liwasilishwe ndani ya miaka miwili tangu ukiukaji kufanyika. (Kanuni za IOWA 792A)

JE, KUNA HAKI NYINGINE?

Kosa la Chuki likifanyika kuhusiana na makazi, ajira, kupata mkopo, makazi ya umma, au elimu, linaweza kuwa suala la ukiukaji wa nidhamu chini ya Kanuni za Haki za Binadamu Jijini IOWA/Mada ya 2 ya Kanuni za Jiji. Malalamiko sharti yawasilishwe ndani ya siku 300.

NJIA 10 ZA KUKABILI CHUKI

CHUKUA HATUA Fanya kitu. Kutochukua hatua chuki inapofanywa kutachukuliwa kuwa kukubali kitendo hicho miongoni mwa wanaokitenda, jamii, na mbaya zaidi, waathiriwa.

UNGANA Mpigie simu rafiki au mfanyakazi mwenza. Andaa kundi la washirika kutoka eneo unapoabudu, shule, vilabu au miungano mingine ya kijamii. Buni muungano wenye watu tofautitofauti

WASAIIDIE WAATHIRIWA Watu wanaoathiriwa na makosa ya chuki wapo katika hatari ya madhara, huhisi hofu na upweke. Hakikisha wanafahamu kwamba unawajali.

CHUNGUZA Bainisha ikiwa kuna kundi la chuki limehusika, fanya utafiti kuhusu alama na ajenda zake. Tafuta ushauri kutoka kwa mashirika ya kupambana na chuki.

USINYAMAZE Hata wewe una Uhuru wa Kujieleza. Chuki inafaa kufichuliwa na kukataliwa.

SHAWISHI VIONGOZI Washawishi viongozi wa siasa, biashara na jamii kukataa chuki.

MKATATI WA MUDA MREFU Buni jumuiya ya "mwitiko chanya". Andaa matukio ya kila mwaka, kama vile matamasha au maonyesho ya tamaduni ili kusherehekea utangamano wa watu mbalimbali.

FUNZA UTANGAMANO Watu hujifunza mitazamo mapema maishani, hasa nyumbani, lakini watoto kutoka jamii mbalimbali wanaweza kuhamasishwa na mitaala na mipango mbalimbali shuleni.

CHUNGUZA ZAIDI Dadisi masuala yote yanayotugawanya. Piga vita ubaguzi katika makao, ajira, maeneo ya makazi ya umma, mikopo na elimu. Jitazame mwenyewe kama una ubaguzi, chuki bila sababu na kasumba.

(Imetayarishwa kutoka kwenye 10 Ways to Fight Hate, a Community Response Guide ya Kituo cha Sheria cha Southern Poverty Law)

Kijitabu hiki ni muhtasari wa jumla wa sheria.



**TUME YA HAKI ZA BINADAMU
JJI LA IOWA**

410 E. Washington St.
Iowa City, IA 52240
www.icgov.org/humanrights
356-5022 au 356-5015
humanrights@iowa-city.org